



JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MJI WA MBULU  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Simu 255 271 2533331  
Barua pepe: td@mbulutc.go.tz

S.L. P 164,  
MBULU-MANYARA

KUMB.NA.MDC/DED/P.2/5/67

27.07.2022

### TANGAZO LA KUITWA KWENYE MAFUNZO

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mbulu anapenda kuwataarifu Waombaji wote walioomba kazi ya Ajira za Muda ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 zilizotangazwa kupitia tangazo la tarehe **05/05/2022** hadi tarehe **19/05/2022** na kusailiwa kuanzia tarehe **19/07/2022** hadi **20/07/2022** kuwa waombaji waliofaulu Usaili wanaitwa kwenye mafunzo tarehe **29/07/2022** kwa ajili ya kutekeleza Zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 katika vituo vilivyoainishwa kwenye Jedwali lililopo hapo chini kuanzia saa **1.30** asubuhi bila kukosa.

Aidha, Mwombaji aliyechaguliwa akikosa kufika katika kituo alichopangiwa kuhudhuria Mafunzo atakuwa amepoteza nafasi yake.

Vituo vya kufanyia Mafunzo vitakuwa kama inavyoonekana katika Jedwali hapo chini.

NA.	KITUO	KATA HUSIKA	MAHALI
1.	JENGO LA MAENDELEO YA JAMII	MARANG, DAUDI, BARGISH, GUNYODA, SILALODA NA IMBORU	UKUMBI WA COMMUNITY CENTRE
2.	CHIEF SARWATT SEKONDARI	GEHANDU, AYAMOHE, UHURU, SANU BARAY, ENDAGIKOT, AYAMAAMI, TLAWI, KAINAM, NAHASEY, NAMBIS NA MURRAY	UKUMBI WA SHULE YA SEKONDARI SARWATT

Aidha, waombaji wote walioitwa kwenye Mafunzo wanapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo:-

- Wafike katika Eneo la Mafunzo kulingana na Kata walizoombea Kazi.
- Kila Mwombaji atajigharamia kwa usafiri wakati anaripoti katika kituo chake cha Mafunzo.
- Kila Mwombaji aliyechaguliwa anapaswa kuwa na Kitambulisho kwa ajili ya Utambuzi. Vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na Kitambulisho cha mkazi, kitambulisho cha Mpiga kura, Kitambulisho cha Uraia au Hati ya kusafiria.
- Mwombaji aliyechaguliwa ambaye hatafika na nyaraka zilizoainishwa hataruhusiwa kuingia kwenye darasa la Mafunzo.
- Mwombaji aliyechaguliwa ambaye hatafika katika Mafunzo atakuwa amepoteza nafasi yake.
- Waombaji ambao majina yao hayajaonekana kwenye orodha iliyoambatishwa pamoja na tangazo hili watambue kuwa hawakukidhi vigezo hitajika.

*Heri A. Kaombwe*  
HERI A. KAOMBWE  
KAIMU MKURUGENZI  
HALMASHAURI YA MJI  
MBULU

**HALMASHAURI YA MJI  
MBULU**

**Nakala:** Mbao za Matangazo  
Mkuu wa Wilaya ya Mbulu  
Watendaji wote wa Kata na Vijiji

- Kwa taarifa  
- Kwa utekelezaji



**Sensa kwa Maendeleo; Jiandae Kuhesabiwa**